**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI.**

**06** **URAIA NA MAADILI**

**Muda: Saa 1:40** **MAJIBU** **Mwaka: 2023**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii in sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali arobaini na tano (45).
2. Jibu maswali yote.
3. Soma maelekezo yote yaliyoko katika **fomu maalumu ya kujibia (OMR)**
4. Jaza taarifa zote katika fomu ya **OMR**

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

***Prepared by Maria Marco for TETEA***

1. Uhuru na umoja wa kitaifa ni mambo ya kujivunia kwa kila mtanzania. Ipi ni athari inayotokana na kuvurugwa kwa uhuru na umoja wa taifa nchini?

   A Kudumaa kwa maendeleo ya nchi

   B Kupungua kwa deni la Taifa

   C Kupungua kwa vitega uchumi

   D Kukosekana kwa utawala bora

   E Kuongezeka kwa rushwa

Jibu sahihi: A Kudumaa kwa maendeleo ya nchi

Sababu: Kukosekana kwa umoja na uhuru husababisha migogoro, uvunjifu wa amani, na hivyo maendeleo hushindwa kupatikana kutokana na ukosefu wa utulivu wa kijamii na kiuchumi.

2. Watu wenye mahitaji maalumu huhisikia vizuri na kujiamini wanapopenda na kuthaminiwa katika jamii. Ni tendo gani linapaswa kuepukwa tunapotoa huduma kwa watu wa kundi hilo?

   A Kuwapa huduma sahihi za afya

   B Kuwachagua katika nafasi za siasa

   C Kuwatenga kwenye nafasi za uongozi

   D Kuwasaidia kwenye masuala ya kisheria

   E Kutumia lugha vizuri

Jibu sahihi: C Kuwatenga kwenye nafasi za uongozi

Sababu: Kuwatenga watu wenye mahitaji maalum ni ubaguzi unaowanyima fursa sawa, hivyo jamii inapaswa kuwajumuisha katika nyanja zote za maisha.

3. Wanafunzi wanapaswa kushirikishwa katika mchakato wa kupanga mipango ya maendeleo ya shule zao. Ni kipengele gani kinapaswa kuonekana kabla ya vingine katika mpango mkakati wa shule?

   A Tathmini

   B Muda

   C Utekelezaji

   D Malengo

   E Mahitaji

Jibu sahihi: E Mahitaji

Sababu: Kabla ya kupanga au kutekeleza mpango wowote, lazima kwanza kubaini mahitaji ya shule ili mipango iwe na msingi sahihi unaolenga kutatua changamoto zilizopo.

4. Ni kiongozi yupi katika muundo wa serikali ya kata ana kazi na wajibu wa kuelimisha jamii dhidi ya tamaduni potofu?

   A Diwani

   B Afisa maendeleo

   C Afisa mtendaji

   D Afisa elimu

   E Afisa afya

Jibu sahihi: B Afisa maendeleo

Sababu: Afisa maendeleo ya jamii anahusika na kutoa elimu na hamasa kuhusu mila na desturi potofu ili kuboresha maisha ya watu katika jamii.

5. Kila shule inahitaji kufanya vizuri kitaaluma. Ni njia ipi inaweza kusaidia shule kufanya vizuri kitaaluma?

   A Kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi shuleni

   B Kuwa na wanafunzi wenye nidhamu

   C Kuwa na idadi kubwa ya watumishi shuleni

   D Kuwaruhusu walimu kushiriki kazi za nje muda wote

   E Kufanya midahalo mara kwa mara shuleni

Jibu sahihi: B Kuwa na wanafunzi wenye nidhamu

Sababu: Nidhamu huwafanya wanafunzi kusoma kwa bidii, kuheshimu walimu, na kutii taratibu za shule, jambo linaloleta mafanikio ya kitaaluma.

6. Ipi kati ya zifuatazo ni sifa nzuri ya shule?

   A Wanafunzi kupewa muda mwingi wa kucheza.

   B Walimu kuonesha nidhamu nzuri.

   C Viongozi wa shule kuwa na uhuru mkubwa.

   D Kutunzwa vizuri kwa mazingira ya shule.

   E Wanafunzi kuvaa wanazozipenda.

Jibu sahihi: D Kutunzwa vizuri kwa mazingira ya shule

Sababu: Mazingira safi na yaliyotunzwa vizuri huongeza ari ya kujifunza na kuleta afya njema kwa walimu na wanafunzi.

7. Kwa nini wanafunzi wanashauriwa kuvaa vizuri kwa kudhihifu shuleni na nyumbani?
   A Ili kuakisi utandawazi
   B Ili kuonesha usasa
   C Ili kuakisi tabia njema
   D Ili kuonesha mitindo ya mavazi
   E Ili kuonesha ufanarhi

Jibu sahihi: C Ili kuakisi tabia njema

Sababu: Mavazi ya heshima huonyesha nidhamu na maadili mazuri kwa mwanafunzi, hivyo hujenga heshima kwake na kwa wengine.

8. Ni shughuli ipi kati ya zifuatazo sio ya kujitolea?
   A Kuanzisha bustani ya mboga
   B Kufagia eneo la shule
   C Kushiriki katika klabu ya skauti
   D Kupanda miti au maua shuleni
   E Kuimba wimbo wa shule

Jibu sahihi: E Kuimba wimbo wa shule

Sababu: Kuimba wimbo wa shule ni utaratibu wa kawaida wa kitaasisi, si tendo la kujitolea, kwani halihusishi kutoa huduma kwa hiari.

9. Utakitajie kitendo cha vijana wengi kushiriki katika majanga ya moto kwa kusaidia kutoketeketea kwa watu, mifugo, majengo na vifaa vingine?
   A Zimamoto
   B Uokoaji
   C Uhoradi
   D Uzalendo
   E Utiifu

Jibu sahihi: B Uokoaji

Sababu: Kushiriki katika kuzuia madhara ya majanga ni tendo la uokoaji, kwa sababu linalenga kulinda maisha na mali za watu.

10. Mahusiano mema katika jamii hujengwa kwa matendo mazuri yanayotendwa na wanajamii. Ni matendo gani yanajenga mahusiano hayo?

    A Uaminifu na ubinafsi

    B Uvivu na ustahimilivu

    C Ukweli na uwazi

    D Uaminifu na umbea

    E Uvumilivu na migogoro

Jibu sahihi: C Ukweli na uwazi

Sababu: Ukweli na uwazi huimarisha uaminifu na kuondoa migongano, hivyo kujenga mahusiano mazuri katika jamii.

11. Vitendo vya kikatili kwa watoto vinaweza kufanyika katika ngazi mbalimbali kwenye jamii. Je, mtoto anawezaje kuepuka vitendo hivyo?

    A Kuwa mpole na mwenyekevu

    B Kuwa mwadilifu na mwangalifu

    C Kuwa mpole na mcheshi

    D Kuwa mchangamfu na mpole

    E Kuwa mstahimilivu na mwadilifu

Jibu sahihi: B Kuwa mwadilifu na mwangalifu

Sababu: Mtoto akiwa mwadilifu na mwangalifu atatambua matendo yasiyofaa na kujiepusha na watu au mazingira hatarishi.

12. Ni muhimu kutenda mambo mema kwa wengine kwa namna ambayo wewe ungependa kutendewa. Kitendo kipi kinaonesha kuwajali wengine?

    A Kumlsha chakula mgonjwa

    B Kuvaa nguo nzuri

    C Kusalimia wazee kwa heshima

D Kuvaa nguo za heshima

E Kucheza pamoja na wengine

Jibu sahihi: A Kumlsha chakula mgonjwa

Sababu: Kumlisha mgonjwa ni kitendo cha huruma na upendo kinachoonyesha kuwajali watu wenye uhitaji.

13. Amani na usalama katika jamii hujengwa kwa maelewano mazuri. Ni mbinu gani inaweza kutumika kujenga uhusiano mzuri na watu wengine katika jamii?

A Kushirikiana wakati wa raha

B Kushirikhana matatizo ya kifamilia

C Kushirikiana wakati wa shida na raha

D Kuwatembelelea ili kujua shida zao

E Kushirikiana wakati wa shida

Jibu sahihi: C Kushirikiana wakati wa shida na raha

Sababu: Kushirikiana katika nyakati zote huonyesha upendo wa kweli na huimarisha uhusiano imara katika jamii.

14. Kundi lipi sio la watu wenye mahitaji maalamu katika jamii?

A Vijana wenye nguvu

B Watu wenye ulemavu wa kusikia

C Watoto wenye ulemavu wa kuona

D Watu wenye ulemavu wa ngozi

E Watu wenye ulemavu wa akili

Jibu sahihi: A Vijana wenye nguvu

Sababu: Watu wenye nguvu na afya njema hawana uhitaji maalumu, tofauti na wale wenye ulemavu wa kiakili, ngozi, au hisia.

15. Ipi ni faida ya matumizi sahihi ya mitandao ya mawasiliano kwenye jamii?

A Hutoa takwimu an taarifa sahihi

B Huheshimu usawa wa binadamu

C Husaidia kufanya miamala ya fedha

D Husaidia kutuma ujumbe sahihi

E Husaidia kutunza siri za watu

Jibu sahihi: C Husaidia kufanya miamala ya fedha

Sababu: Mitandao ya mawasiliano inarahisisha huduma kama benki mtandao, malipo ya simu, na biashara mtandaoni kwa ufanisi.

16. Ili nchi iendelee, inahitaji uongozi bora. Sifa ipi inapambanua kiongozi bora katika jamii?

A Kupendwa na watu

B Kuwa mzungumzaji sana

C Kutimiza wajibu

D Kuwa na uwezo wa kifedha

E Kuwa na elimu ya juu

Jibu sahihi: C Kutimiza wajibu

Sababu: Kiongozi bora ni yule anayetekeleza majukumu yake kwa uadilifu, uwajibikaji, na kujali maslahi ya wananchi.

17. Muda ni miongoni mwa rasilimali zinazoangia katika maendeleo endelevu. Je, nini kinahitajika ili kutumia muda vizuri?

A Kupangilia matukio kulingana na fursa

B Kupangilia mambo yajayo kwa kuangalia rasilimali

C Kupangilia majukumu kulingana na rasilimali zilizopo

D Kupangilia mambo yajayo kwa kuzingatia fedha

E Kupangilia matukio kulingana na vipaumbele

Jibu sahihi: E Kupangilia matukio kulingana na vipaumbele

Sababu: Kupangilia mambo kwa kuzingatia umuhimu wake husaidia kutumia muda kwa ufanisi na kuepuka kupoteza muda.

18. Rasilimali za shule zinaweza kutumika kuleta maendeleo, na ni wajibu wa kila mmoja kuzilinda. Hatua zipi zinatakiwa kuchukuliwa katika kufanya utunzaji wa rasilimali hizo?

A Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara

B Kufanya ukaguzi na kutoa taarifa

C Kufanya ukaguzi na kuzigawa rasilimali kwa watu

D Kufanya ukaguzi na kununua rasilimali mpya

E Kufanya ukaguzi na kuzitupa

Jibu sahihi: B Kufanya ukaguzi na kutoa taarifa

Sababu: Kufanya ukaguzi na kutoa taarifa husaidia kubaini matumizi sahihi ya rasilimali na kuchukua hatua za marekebisho mapema.

19. Matendo yafuatayo hujenga nidhamu binafsi kwa wanafunzi isipokuwa:

A kumaliza kazi kwa wakati.

B Kuwa na ratiba ya kujisomea.

C kusoma kwa bidii.

D kutumia muda vizuri.

E kusubiri kupangiwa majukumu.

Jibu sahihi: E kusubiri kupangiwa majukumu

Sababu: Kusubiri kupangiwa majukumu kunapunguza uwajibikaji binafsi na kutojenga nidhamu ya kujitegemea.

20. Rushwa imekuwa kikwazo kikubwa katika maendeleo ya nchi. Ni njia ipi kati ya hizi zifuatazo sio ya kuzuisia na kupambana na rushwa nchini?

A Uwazi

B Uzalendo

C Uadilifu

D Ustahimilivu

E Uwajibikaji

Jibu sahihi: D Ustahimilivu

Sababu: Ustahimilivu ni uvumilivu, si njia ya kupambana na rushwa, wakati uwazi na uadilifu vinasaidia kuzuia vitendo hivyo.

21. Tendo lipi linaonesha uwepo wa utawala bora katika ngazi ya familia?

A Kununulia familia nguo nzuri na za kisasa

B Kuhakikisha kuwa wanafamilia wote wanapata haki sawa

C Uwepo wa chakula kitamu kwa wanafamilia

D Uwepo wa samani nzuri na za gharama nyumbani

E Watoto kuwa huru kuchagua marafiki

Jibu sahihi: B Kuhakikisha kuwa wanafamilia wote wanapata haki sawa

Sababu: Utawala bora unahusisha usawa, haki, na ushirikishwaji wa kila mwanafamilia katika maamuzi na fursa.

27. Utakapoaanzsa masomo ya sekondari Kidato cha Kwanza mwaka 2024, ni aina ipi ya wanafunzi unapaswa kushirikiana nao unapokuwa shuleni?

A Wenye utiifu kwa viongozi wa shule

B Wenye ujuzi wa kucheza michezo mbalimbali

C Wasomaji wa vitabu vingi

D Wenye nidhamu nzuri

E Wenye kujiamini wakati wote

Jibu sahihi: D Wenye nidhamu nzuri

Sababu: Nidhamu nzuri hujenga ushirikiano, kuheshimiana, na mazingira bora ya kujifunzia. Wanafunzi wenye nidhamu huwasaidia wengine kufuata taratibu na kuzingatia malengo ya kielimu.

28. Ng'ombe wa Bwana Ngumvali walikufa kutokana na ukame. Bwana Ngumvali aliamua kuiba ng'ombe wa Bwana Kazimolo. Ni tabia ipi Bwana Ngumvali alishindwa kuionesha?

A Uwajibikaji na uvumilivu

B Uvumilivu na wizi

C Uvumilivu na uadilifu

D Uadilifu na ustahimilivu

E Uvumilivu na ukarimu

Jibu sahihi: C Uvumilivu na uadilifu

Sababu: Bwana Ngumvali hakusubiri suluhisho la halali bali alichukua mali ya mtu mwingine. Kitendo hicho kinaonyesha kukosa uvumilivu na uadilifu kwa kuwa aliendа kinyume na maadili ya uaminifu.

29. Kila mtu ana majukumu ya kutekeleza katika jamii. Jukumu gani kuu wanafunzi wanatakiwa kulitekeleza shuleni?

A Kusoma masomo yote kwa bidii

B Kushiriki katika michezo shuleni

C Kukimbia mchakamchaka

D Kumwagilia bustani ya shule

E Kusafisha eneo la shule

Jibu sahihi: A Kusoma masomo yote kwa bidii

Sababu: Kazi kuu ya mwanafunzi ni kujifunza na kufanya vizuri kitaaluma. Bidii katika masomo ndiyo msingi wa mafanikio shuleni na katika maisha ya baadaye.

30. Ni muhimu sana kwa wanafunzi kutekeleza majukumu ya nyumbani. Ni kwa namna gani wanafunzi wanaweza kuongeza ufanisi katika utendaji wa shughuli za nyumbani?

A Kutumia ratiba ya shuleni kufanya shughuli za nyumbani

B Kufanya kazi kwa bidii shuleni tu

C Kutokwenda shule hadi akamilishe shughuli zote za nyumbani

D Kufanya tathmini ya utendaji wa majukumu yote ya nyumbani

E Kufanya majukumu ya nyumbani usiku kucha

Jibu sahihi: D Kufanya tathmini ya utendaji wa majukumu yote ya nyumbani

Sababu: Kufanya tathmini humsaidia mwanafunzi kujua kazi zilizofanyika vizuri na zile zinazohitaji kuboreshwa, hivyo kuongeza ufanisi na uwajibikaji.

31. Babulee alikataa kwenda kuwinda ndege na rafiki zake kwa kuwa ulikuwa muda wa kipindi cha Hisabati. Alipouliuzwa alijibu kwamba alipima faida na hasara za jambo hilo ndipo alifanya uamuzi. Kitendo hiki kinaitwaje?

A Tathmini ya kina

B Mawazo ya kina

C Uamuzi sahihi

D Mapendekezo sahihi

E Uchambuzi wa kina

Jibu sahihi: C Uamuzi sahihi

Sababu: Babulee alitumia busara na kutathmini athari za kitendo kabla ya kuchukua hatua. Hivyo alifanya uamuzi sahihi kwa kuzingatia manufaa ya elimu.

32. Tabia ya unafiki katika jamii ni jambo lisilo faa kutokana na athari zake hasi. Kipi kifanyike ili kuiondoa katika jamii?

A Kushitaki wanafiki mahakamani

B Kuhoji wanafiki mbele ya umma

C Kueleza ukweli kuhusu unafiki

D Kusuta wanafiki mbele ya umma

E Kuwatenga wanafiki na watu wengine

Jibu sahihi: C Kueleza ukweli kuhusu unafiki

Sababu: Elimu na ukweli huondoa unafiki kwa kuwafanya watu watambue madhara yake na kuacha tabia hiyo. Ukweli hujenga uaminifu katika jamii.

33. Rushwa ni adui wa haki za watu na maendeleo. Madhara ya rushwa katika jamii ni yapi?

A Kupata wataalamu wasio na sifa

B Kupata wahitimu wengi

C Kushuka kwa bei za bidhaa

D Kushuka kwa idadi ya vifo

E Kukosekana kwa matabaka katika jamii

Jibu sahihi: A Kupata wataalamu wasio na sifa

Sababu: Rushwa husababisha watu wasiostahili kupata nafasi, hivyo jamii hupata viongozi au wataalamu wasio na uwezo wa kufanya kazi kwa ufanisi.

34. Ukweli na uwazi ni tabia muhimu katika jamii, ingawa baadhi ya wanajamii huzipuuza. Njia zipi zitumike ili kuboresha tabia hizi?

A Kushauri watu kuwa wastahimilivu na wanyenyekevu

B Kuwaelekeza watu kuongea ukweli na kukataa maovu

C Kusisitiza uaminifu kwa viongozi

D Kufuata mawazo ya wazee katika jamii

E Kufuata miongozo ya viongozi waliopo

Jibu sahihi: B Kuwaelekeza watu kuongea ukweli na kukataa maovu

Sababu: Kufundisha na kusisitiza ukweli na kupinga maovu hujenga uwazi na uadilifu katika jamii, hivyo kuboresha tabia hizo.

35. Tanzania inasifika kwa kuwa na uhusiano mzuri na mataifa mengine. Ipi ni misingi ya Tanzania kuhusu sera ya mambo ya nje?

A Usawa na utu

B Uhuru na ujamaa

C Uwazi na ukweli

D Mshikamano na uvumilivu

E Uhuru na kujitegemea

Jibu sahihi: E Uhuru na kujitegemea

Sababu: Sera ya mambo ya nje ya Tanzania imejikita katika misingi ya uhuru, amani, na kujitegemea kama urithi kutoka kwa Azimio la Arusha na falsafa ya Mwalimu Nyerere.

36. Umoja wa Mataifa ni chombo kinachojumuisha mataifa huru duniani. Jambo gani lilichangia kuanzishwa kwake?

A Kuzuia Marekani isitawale dunia

B Kuepusha vita nyingine ya dunia isitokee

C Kuandaa mataifa ya Afrika kupata uhuru wao

D Kulinda maslahi ya nchi tajiri duniani

E Kuzuia Uingereza isitawale mataifa ya kiafrika

Jibu sahihi: B Kuepusha vita nyingine ya dunia isitokee

Sababu: Umoja wa Mataifa (UN) ulianzishwa mwaka 1945 baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia ili kudumisha amani, haki, na ushirikiano kati ya mataifa huru duniani.

37. Ni mila ipi potofu humsababishia mamajmi mzito kutoka damu nyingi au kupoteza maisha wakati wa kujifungua?

A Kuzuia wanawake kula baadhi ya vyakula

B Ukeketaji kwa wanawake

C Mwanamke kufanya kazi nyingi

D Kuwa na jukumu la kuhudumia familia

E Kurithi wajane

Jibu sahihi: B Ukeketaji kwa wanawake

Sababu: Ukeketaji ni mila hatarishi inayosababisha majeraha, maambukizi, na wakati mwingine kifo kutokana na kutokwa damu nyingi au maumivu makali wakati wa kujifungua.

38. Tanzani ni mwanachama wa jumuhiya ya madola. Jumuiya hiyo inaundwa na wanachama walio watawaliwa na nchi gani?
    A Ufaransa
    B Uingereza
    C Ureno
    D Ubelgiji
    E Ujerumani

Jibu sahihi: B Uingereza

Sababu: Jumuiya ya Madola inaundwa na nchi zilizowahi kuwa chini ya utawala wa Uingereza kabla ya kupata uhuru, ikiwemo Tanzania.

39. Kuchangamana na watu wenye tamaduni na asili tofauti ni jambo la msingi kwa nchi yoyote. Kuna umuhimu gani wa kuishi na watu wenye asili tofauti?
    A Wanatuwezesha kubadilishana ujuzi
    B Wanatisaidia kupuuza tamaduni za kigeni
    C Wanatusaidia kulinda uzalendo wetu
    D Wanatuwezesha kusahau historia za kigeni
    E Wanatuhamasisha kulinda tamaduni za asili

Jibu: A Wanatuwezesha kubadilishana ujuzi

Sababu: Kuishi na watu wenye tamaduni tofauti kunatoa fursa ya kubadilishana maarifa na ujuzi tofauti. Hii inasaidia kujifunza mbinu mpya, mitazamo mbalimbali, na uzoefu wa kipekee kutoka kwa wengine, jambo ambalo linaimarisha maendeleo ya kijamii na kitaaluma. Chaguzi nyingine hazionyeshi faida ya moja kwa moja ya kubadilishana ujuzi.

40. Njia ipi inaweza kutumika katika kukabiliana na madhara hasi ya utandawazi nchini Tanzania?
    A Kuwasikiliza wazazi na kulinda utamaduni wetu
    B Kuzikubali tamaduni zingine na kulinda uzalendo wetu
    C Kutumia mitandao ya kijamii bila usimamizi

D Kukuza teknolojia ya mawasiliano kutoka nchi zilizoendelea

E Kuhamasisha vijana kuacha kutumia mitandao ya kijamii

Jibu: B Kuzikubali tamaduni zingine na kulinda uzalendo wetu

Sababu: Kukabiliana na madhara hasi ya utandawazi kunahitaji mchanganyiko wa kukubali tamaduni za kigeni huku tukihifadhi uzalendo na tamaduni zetu. Njia hii inazuia kupoteza utambulisho wa kitaifa na husaidia watu kuishi kwa amani na kushirikiana na watu wa tamaduni tofauti. Chaguzi C, D, na E hazitatua madhara ya utandawazi kwa njia yenye manufaa ya kudumu, na chaguo A linashughulikia zaidi heshima kwa wazazi kuliko utandawazi kwa ujumla.

41. Uhusiano wa kidiplomasia kati ya Tanzania na nchi nyingine hutoa fursa mbalimbali. Fursa zipi mbili zinapatikana kutokana na uhusiano huo?

**Uhusiano wa kidiplomasia unarahisisha biashara na uwekezaji wa kimataifa, jambo linalosaidia kuinua uchumi wa nchi.**

**Unakuza ushirikiano wa kisiasa na kijamii, kwa mfano kushirikiana katika masuala ya elimu, afya, na maendeleo ya kiufundi, jambo linaloongeza fursa za kujifunza na kubadilishana uzoefu.**

42. Pazi ni mwanafunzi mwenye tabia ya kukiuka sheria za shule. Je, ni madhara gani mawili yanaweza kumpata?

**Pazi anaweza kupokea adhabu ya kisheria au ya shule kama vile kusimamishwa au kupewa kazi za ziada za shule, jambo linalofundisha kufuata sheria.**

**Tabia yake inaweza kuathiri sifa yake na mahusiano na walimu na wanafunzi wenzake, jambo linaloweza kumfanya ashindwe kushirikiana na wengine kikamilifu.**

43. Vyanzo gani viwili vinaweza kutumika katika kupokea na kutoa taarifa sahihi shuleni?

**Vitabu vya shule na makala rasmi kutoka vyombo vya elimu vinatoa taarifa sahihi na zinazothibitishwa.**

**Walimu na viongozi wa shule wanaweza kutoa taarifa sahihi kwa njia ya mihadhara, mikutano, au onyo la moja kwa moja, kwani wanafahamu sera na miongozo ya shule.**

44. Njia zipi mbili zinaweza kutumika kuondoa changamoto ya miundombinu chakavu na mrundikano wa kesi mahakamani kwa lengo la kusaidia mahakama kufikia malengo yake?

**Kuboresha na kudumisha miundombinu ya mahakama kama majengo, vifaa, na teknolojia ya kielektroniki kunapunguza msongamano wa kesi na kufanya kazi ya mahakama iwe rahisi.**

**Kuanzisha mfumo wa usimamizi wa kesi kwa kutumia teknolojia ya kisasa (kama usajili wa kesi mtandaoni) kunarahisisha kufuatilia kesi na kuharakisha ufungaji wa kesi.**

45. Kwa nini jumuiya za kiuchumi katika Bara la Afrika hazijafikia malengo yaliyotarajiwa? Toa sababu mbili.

**Migogoro ya kisiasa na ukosefu wa mshikamano miongoni mwa nchi wanachama inazuia utekelezaji wa sera za jumuiya kwa usahihi.**

**Miundombinu duni ya barabara, nishati, na mawasiliano inakwamisha biashara na ushirikiano wa kiuchumi, jambo linalopunguza faida za jumuiya hizo.**